# JARIBIO LA MTIHANI

## DARASA LA NANE - MWAKA 2020

STEP FLYER SERIES — STEP FLYER (002)

# KISWAHILI:LUGHA

(8)

**SEHEMU YA KWANZA :LUGHA**

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

***Muda: Saa 1 Dakika 40***

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Kuku ____1____ ____2____ waliaga dunia ____3____ na maradhi ____4____ kaputula. Kuku ____5____ walianza kufa ____6____ baada ya ____7____ . Halafu ya kitambo ____8____ , kizimba ____9____ kikabaki tupu. Ni kuku ____10____ hao tuliowategemea____11____ karo. Tulijiuliza,"Tutaishi____12____ ?" Hata hivyo hatukujua ____13____ tungesubiri siku ____14____ kabla ya kupata ____15____ .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. wetu | B. zetu | C.vyetu | D.kwetu |
| 2. | A.zote | B.wote | C.kwote | D.vyote |
| 3. | A.kutoka | B.kutokwa | C.kutokana | D.kutokea |
| 4. | A.za | B.na | C.cha | D.ya |
| 5. | A.zenyewe | B.mwenyewe | C.kwenyewe | D.wenyewe |
| 6. | A.mojamoja | B.moja | C.mmoja | D.mumoja |
| 7. | A.wengine | B.mwingine | C.ingine | D.nyingine |
| 8. | A.kidogo | B.mdogo | C.kudogo | D.dogo |
| 9. | A.nacho | B.ndicho | C.sicho | D.nayo |
| 10. | A.wawo | B.ao | C.wao | D.wawa |
| 11. | A.wa | B.za | C.kwa | D.na |
| 12. | A.wapi | B.kupi | C.mpi | D.vipi |
| 13. | A.kua | B.kuamba | C.kuwa | D.vile |
| 14. | A.ngapi | B.gani | C.zipi | D.ipi |
| 15. | A.mpya | B. wapya | C.vipya | D.kupya |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Mtoto anayezaliwa katika ndoa baina ya Mzungu na Mwafrika huitwaje?

A. mjolo B. suriama
C. kitimbakwiri D. chotara

**17.** Jina jingine la ***msichana*** ni


A. banati B. mvuli
C. barobaro D. ghulamu

**18.** ***Tambua maana ya sentensi hii:***

Nilimwua simba seuze kuku.

A. kwa kuwa alimwua simba,kuku hataepuka
B. kwa kuwa alimwua simba,kuku hana bahati
C. ikiwa alimwua simba, hawezi kushindwa kumwua kuku
D. ikiwa atamwua simba,kuku awe tayari

**19.** Jina la umbo hili ni;



A. tao B. hilali
C. kipenyo D. tao

**20.** ***Andika tarakimu ifuatayo kwa maneno***:

404, 404

A. Arubaine elfu na nne mia nne na nne
B. Mia nne elfu na nne na arubaine na nne
C. Laki nne na nne elfu, mia nne na nne
D. laki mia tatu na tatu elfu, na mia tatu na tatu

**21.** Neno ***kiwete*** liko katika ngeli gani?

A. A- WA B. KI - VI
C. I - ZI D. U - YA

**22.** ***Kanusha sentensi hii;***

***Mto ambao ulifurika umefungwa***

A. Mto ambao ulifurika haujafungwa
B. Mto ambao haukufurika haujafungwa
C. mto ambao haujafurika haukufungwa
D. mto ambao haujafurika haujafungwa

**23.** Akisami $^3/_4$ ni

A. humusi nne B. theluthi tatu
C. thumni nne D. robo tatu

**24.** ***Umoja wa sentensi hii ni:***

***Kwato za ng'ombe wale zina mipauko***

A. Ukwato wa ng'ombe zile una mipauko
B. Ukwato wa ng'ombe yule una mipauko
C. Ukwato wa ng'ombe yule una mpauko
D. Kwato za ng'ombe yule zina mipauko

**25.** ***Sabalkheri*** ni salamu ya wakati gani?

A. Jioni B. Adhuhuri
C. Asubuhi D. Usiku

**26.** Sehemu inayohifadhi mkojo mwilini huitwa?

A. nswi B. figo
C. pafu D. kibofu

**27.** Unda nomino dhahania kutokana na kitenzi ***remba.***

A. mrembo B. urembo
C. kirembo D. marembo

**28.** Kimatu ni kwa nzige kama vile _____ ni kwa nyuki.

A. jana B. kiluwiluwi
C. kihongwe D. kisui

**29.** Nyana zinazoshikilia nyama kinywani huitwa:

A. kiga B. sarara
C. fizi D. pakacha

**30.** Mke na dada wa mume huitana:

A. mwanyumba B. mitara
C. shemeji D. wifi

**_Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali kutoka 31 - 40._**

Kunguru aliugua <u>maradhi</u> mabaya kwa muda mrefu. Alikonda sana. Hakuwa na nguvu za kutafuta chakula. Njaa ilimuuma si haba. Hakujua jinsi ya kutafuta chakula kwani ubongo wake haungefikiria vizuri.

Nyumbani kwake kulikuwa na nyasi nyingi sana ndefu. Huko kulijaa panzi lakini kunguru hangeweza kuwadona kwa sababu walitoroka. Panzi walimcheka kunguru mnyonge kwa! kwa ! kwa! kunguru alipokuwa akitembea siku moja aliwaona panzi wawili wakipigana kufa na kupona. Baadaye waliaga dunia, baada ya kuumizana na kupata majeraha mabaya sana.

Kunguru alitoka pahali alikuwa na kuwadona. Aliwala. Walikuwa watamu ajabu. Alijaribu kutafuta panzi wengine waliokuwa wamekufa kwa sababu hakushiba. Hakufanikiwa hata kidogo.

Aliamua kuwachochea panzi. Alitumia panzi mmoja mlafi kwa kumdanganya ati alikula nyasi mbovu ilhali wengine walikula nyasi nzuri. Panzi mlafi alienda na akaanza kutoa fujo kwa panzi wengine. *Vita vilizuka* baina ya panzi. Kunguru alikuwa mbali akicheka na kusema, "wajinga ndio waliwao."

Panzi wengi walikuwa sana kutokana na vita vile, karibu wamalizane. Kunguru alizidi kuchochea panzi kuuana akijifanya rafiki aliyekuwa na hofu zaidi. Baada ya panzi wengi kufa, waliamua kumaliza vita ili wasimalizane. Baada ya vita, kunguru alionekana akiwala mizoga ya panzi waliokufa kwa furaha sana. Panzi walipoona hivyo walijua kunguru ni mwongo.

**31.** Kunguru alikonda kwa nini?
A. Aliugua muda mrefu
B. Hakutaka kula
C. Hakuwa na hamu ya kula
D. Hakukuwa na panzi

**32.** Kwa nini kunguru hakujua jinsi ya kupata chakula?
A. Aliwatafuta panzi
B. Alikuwa peke yake
C. Hakuwa na nguvu
D. Alikosa kufikiria barabara

**33.** Kwa nini kunguru alitamani kuwala panzi wengine?
A. Panzi walikufa zaidi
B. Ni watamu sana
C. Hakushiba
D. Ili awe na nguvu

**34.** Kunguru alipowatafuta panzi wengine:
A. hakuwapata  B. aliwapata
C. alichoka  D. walitoroka

**35.** Kisawe cha neno maradhi ni
A. ugonjwa  B. afya
C. njaa  D. unyonge

**36.** Kusema vita vilizuka ni kusema kwamba
A. vita viliendelea
B. vita vilianza
C. vita vilikoma
D. vita vilimalizwa

**37.** Mnyama akiaga huitwa mzoga je binadamu akiga huitwa?
A. mzogo  B. mtu
C. maiti  D. mfu

**38.** Kunguru alitumia mbinu gani kupata chakula?
A. Kutafuta panzi waliokufa
B. Alichochea vita kwa panzi
C. Alienda hospitalini
D. Aliwinda panzi na akala nyasi

**39.** Panzi waliamua kumaliza vita wakati gani?
A. walipochoka kupigana
B. kunguru alipowacheka
C. walipouana sana
D. walipojua ulikuwa uwongo wa kunguru

**40.** Kichwa kifaacho habari hii ni
A. vita vya panzi furaha ya kunguru
B. uongo wa kunguru
C. panzi watamu
D. kunguru mgonjwa

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Haki ni jambo ama kitu anachostahili mtu kupata. Aidha ni utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo. Kila binadamu ana haki zake za kimaisha. Binadamu ana haki ya chakula, makao, ulinzi na hata mapenzi.

Tuangazie haki za mwananchi wa nchi iliyo huru kama hii yetu ya Kenya. Jambo la kwanza ni uhuru wa kuabudu. Kila mwananchi ana uhuru wa kufanya ibada mahali anapotaka, jinsi anavyotaka na wakati wowote anaotaka. Itiliwe maanani kuwa hana cha kugwaya kuhusu wakati wa ibada kwani wakati wa kuabudu ni yeye mwenyewe wa kuamua.

Haki ya pili ni kukutana. Mwananchi ana haki ya na yeyote ama wowote anaotaka kukutana nao, mahali popote na wakati wowote almuradi wajulishe walinda usalama ili awe na uhakika wa usalama wake. Hata hivyo, anapofanyiwa haki na kuruhusiwa kukutana, naye asiwe mwenye kiburi kama cha mende kutaka kukutana na kupanga maovu dhidi ya wenzake ama hata nchi yake. Aelewe kuwa ada ya mja hunena muungwana ni kitendo.

Haki nyingine ni usalama. Raia wa nchi yoyote ana haki ya kulindwa wakati wote akiwa katika shughuli zake maadamu zisiwe shughuli za uhalifu.

---

**41.** Kwa mujibu wa kifungu, haki si
A. jambo analostahili mtu
B. uborongaji wa taratibu
C. utumiaji bora wa kanuni
D. ufuataji wa sheria

**42.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza, ni ipi isiyokuwa haki ya binadamu?
A. chakula B. maskani
C. maovu D. mapenzi

**43.** Wananchi wanapokuwa katika hali ya wasiwasi kwa sababu ya ujambazi huwa hawana haki ya
A. makutano B. ulinzi
C. kuabudu D. kujieleza

**44.** Mwandishi anasema nini kuhusu uhuru wa kuabudu?
A. Ni kupangiwa mambo yote yanayohusu ibada
B. Nikuchaguliwa mahali pa kuabudu
C. Ni kupewa mwongozo wa jinsi ya kuabudu
D. Ni kuwa na mamlaka ya kuamua mambo yote yanayohusu ibada

**45.** Ikiwa katika nchi iliyo huru serikali itatoa mwongozo wa wakati wa watu kuabudu
A. itakuwa inawapokonya haki ya makutano.
B. itakuwa inawapokonya haki ya mavazi.
C. itakuwa inawapokonya haki ya kuabudu.
D. itakuwa inawapokonya haki ya ushirika.

**46.** Miongoni mw amambo yanayojitokeza katika haki ya kuabudu si pamoja na:
A. maenezi ya porojo
B. jinzi ya kuabudu
C. mahali pa kuabudia
D. wakati wa ibada

**47.** Neno ***almuradi*** lilivyotumika ni aina ya:
A. kihisishi B. kihusishi
C. kiwakilishi D. kiunganishi

**48.** Katika kufurahia uhuru wa kukutana jambo la busara ni:
A. kuwaudhi walinda usalama
B. kuwapuuza walinda usalama
C. kuwataarifu walinda usalama
D. kuwakejeli walinda usalama

**49.** Naye anayetendewa haki asiwe mwenye ***kiburi kama cha mende*** ndiko kusema
A. asifanye uungwana
B. asifanye ujefule
C. asifanye ya utu
D. asifanye ya chuki

**50.** Kwa mujibu wa makala, jukumu la usalama ni la nani?
A. serikali iliyo mamlakani
B. serikali ya upinzani
C. wananchi watukutu
D. wafanyabiashara